

SW
◎ Kiswahili
III 4
☞ Catherine Greenewald
✎ Violet Otiemo
☞ Brigid Simiyu



Likizo kwa bibi

This work is licensed under a Creative Commons




<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>
Attribution 4.0 International License.

☞ Catherine Greenewald
✎ Violet Otiemo
☞ Brigid Simiyu

Global Storybooks
globaletorybooks.net
Likizo kwa bibi






Odongo na Apiyo waliishi mjini na baba yao. Walisubiri likizo kwa hamu. Siyo tu kwa shule kufungwa, bali ni kwa sababu walienda kumtembelea bibi yao. Aliishi katika kijiji cha uvuvi karibu na ziwa kubwa.

Odongo na Apayo walichangamka kwanzi
ulikuwa wakati wa kumtembelea bibi kwa
mara nyiningine. Usiku huo, walipanga
mizigo yao na kujiandaa kwa safari ndefu
ya kwenda kijivini. Hawakuwenza kujala ila
waliongea usiku kuchaa juu ya likizo yao.






Mapema asubuhi iliyofuata, waliondoka katika gari la baba yao kuelekea kijijini. Walipita milima, wanyama pori na mashamba ya majani ya chai. Walihesabu magari na kuimba nyimbo.





Odongo na Apiyo waliporudi shulenii, waliwasimulia marafiki zao kuhusu maisha ya kijijini. Baadhi ya watoto waliamini kuwa maisha ya mjini ni mazuri. Wengine waliamini kijijini ni bora zaidi. Lakini zaidi ya yote, kila mmoja alikubali kwamba Odongo na Apiyo walikuwa na bibi wa kipekee.

Baada ya muda, wato to walichoka na
kusinza.



Odongo na Apayo walimkumbatia kwa
pamoga na kumuaga.







Baba aliwaamsha Odongo na Apiyo walipofika kijijini. Walimkuta bibi yao, Nyar-Kanyada, akipumzika kwenye mkeka chini ya mti. Kwa Dholuo, Nyar-Kanyada maana yake ni 'binti wa watu wa Kanyada'. Alikuwa ni mwanamke mrembo na imara.




Baba yao alipokuja kuwachukua, hawakutaka kuondoka. Walimuomba Nyar-Kanyada aende nao mjini. Alitabasamu na kusema, "Nimezeeka, siyawezi ya mjini. Nitasubiri mje kijijini kwangu tena."


Likizo ilikaribia kuisha na watoto
waliatakiwa kurudi mjinji. Nyar-Kanyada
alimpa Odongo kofia na Apoyo sweta.
Aliwafungia chakula cha kula safariini.

Nyar-Kanyada aliwakaribisha ndani kwa
kuchenza na kumiba kwa furaha. Wajukuu
wake walikuwa na shauku ya kumpa
zawadi walizomletea kutoka mjinji. "Funiga
yangu kwanza," Odongo alisema. "Hapana,
yangu kwanza!" Apoyo akasema.





Baada ya kufungua zawadi, Nyar-Kanyada
aliwabariki wajukuu wake kitamaduni.





Mwisho wa siku walikunywa chai pamoja.
Walimsaidia bibi yao kuhesabu pesa
alizozipata.

Kisha Odongo na Apayo wakende nje.
Walwakimbiza vipepeo na ndege.




Siku nyingine watoto walikwenda sokoni
pamoga na Nyar-Kanyada. Nyar-Kanyada
alikuwa na kibanda cha kuza mboga,
sukari na sabuni. Apayo alipenda kuwatilia
wateja bei za bidhaa. Odongo alifungia
wateja bidhaa walizonuna.







Walipanda kwenye miti na kurushiana maji ziwani.




Asubuhi moja, Odongo aliwapeleka ng'ombe wa bibi yake malishoni. Wakakimbilia ndani ya shamba la jirani. Mwenye shamba alikasirishwa sana na Odongo. Akatishia kuwazuia ng'ombe kula mimea yake. Tangu siku hiyo, Odongo alihakikisha kwamba ng'ombe hawaingii matatani tena.

Nyar-kanyada aliwafundisha wajukuu
wake jinsi ya kupika ugali mwepesi wa kula
na mchuzi. Alivaoresha namna ya kupika
wali wa nazi wa kuliwa na samaki wa
kukangaa.

Giza Iilipointiga, walirudi nyumbani kwa ajili
ya chakula cha jioni. Kabla hata ya
kumaliza kula, walikuwa wanasiizia!





Siku iliyofuata, baba yao alirudi mjini na kuwaacha na Nyar-Kanyada.



Odongo na Apiyo walimsaidia bibi yao na kazi za nyumbani. Walichota maji na kuokota kuni. Walikusanya mayai ya kuku na kuchuma mboga za majani kutoka kwenye bustani.